

**TAARIFA KWA UMMA**

**KURUHUSU UAGIZAJI, USAMBAZAJI, UZAJI NA MATUMIZI YA DAWA YA KUTIBU MALARIA YA VIDONGE YA *METAKELFIN* KUTOKA KAMPUNI YA *PFIZER INC. N/Y* INAYOTENGENEZWA NA KIWANDA CHA DAWA CHA *PHARMACIA & UPJOHN* CHA ITALIA**

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na.1 ya mwaka 2003. Mamlaka ina jukumu la kudhibiti ubora na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ili kulinda afya za watanzania.

Mamlaka ya Chakula na Dawa inapenda kuutaarifu umma kuwa baada ya kufanya tathmini ya maboresho/mabadiliko katika paketi ya dawa ya kutibu Malaria ya *Metakelfin* yaliyofanywa na mtengenezaji wa dawa hiyo imeridhia kurejeshwa katika soko kwa dawa ya *Metakelfin* nchini.

Idhini ya kurejesha dawa hii katika soko inafuatia maamuzi ya TFDA ya kusitisha uagizaji, usambazaji, uzaji na matumizi yaliyotolewa tarehe 21/4/2009 kufuatia kuwepo kwa dawa ya aina hiyo hiyo katika soko yenye kiwango kidogo cha dawa na pia dawa bandia kiasi kwamba haikuwa rahisi kuzitofautisha na dawa halisi.

Maelezo ya ziada ya dawa hiyo: *Metakelfin* iliyorejeshwa sokoni ina viambata hai vya *Sulphamethopyrazine 500mg* na *Pyrimethamine 25mg* na imefungashwa katika pakiti yenye ujazo wa vidonge 30 vilivyofungwa ndani *blisters*/makasha ya vidonge sita (6) na pia maelezo ya matumizi yapo katika lugha ya Kiingereza na Kifaransa. Aidha toleo la dawa (batch No.), tarehe ya kutengeneza na kuisha muda wa matumizi yameandikwa kwa muhuri wa moto. Kasha la nje lina rangi nyeupe na bluu na lina alama ya usalama (security mark) iliyoandikwa *Pfizer* alama hiyo hubadilika rangi unapoiangalia katika pande tofauti. Dawa hii inatengenezwa na kiwanda cha *Pharmacia & Upjohn, Italy S.p.A. Ascoli Piceno* cha Italia chini ya idhini ya *Pfizer inc. N/ Y.*

Mamlaka inapenda kuisitiza kuwa matumizi ya *Metakelfin* ni kwa ajili ya kinga kwa kina mama wajawazito kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Taifa wa Uchunguzi na Tiba ya Malaria wa mwaka 2006 (National Guidelines for Malaria Diagnosis and Treatment 2006).

Imetolewa na

**KAIMU MKURUGENZI MKUU,  
MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA),  
BARABARA YA MANDELA, MABIBO-EXTERNAL,  
S.L.P 77150, DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 222 450512/450751/452108  
Nukushi: +255 222 450793  
Barua Pepe: [info@tfda.or.tz](mailto:info@tfda.or.tz); Tovuti: [www.tfda.or.tz](http://www.tfda.or.tz)**